**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TINDE,<br>
S.L.P. 846,<br>
SHINYANGA.<br>
03/05/2026.

**Namba za Simu:**
Mkuu wa shule: 0756824083
Makamu Mkuu wa Shule: 0753336047
Mwalimu wa Malezi: 0766712219

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**…………………………………………….**
S.L.P……………….
…………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TINDE, HALMASHAURI YA SHINYANGA, MWAKA 2026/2027**

## 1. UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii, mwaka **2026/2027** tahasusi ya…………………..Shule iko umbali wa **kilomita 37** kutoka Shinyanga mjini, eneo la njia panda iendayo Nzega na Kahama kutokea Shinyanga mjini. Kwa wanaotokea maeneo ya Mwanza/Musoma, yapo mabasi yanayotokea Jijini Mwanza (Nyegezi Stand) kuelekea Nzega/Kahama kwa kupitia Tinde ulipo mzani wa kupima uzito wa magari, **hapo ndipo mahali shule hii ilipo**. Pia kuna magari madogo (Noah/Hiace) kutokea Shinyanga mjini hadi Tinde, nauli ni **Tsh. 4,000**/=. Kwa watokao Tabora, Singida, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro na Dar es salaam mabasi yatakufikisha Tinde yakielekea Kahama, Shinyanga mjini hadi Mwanza Jijini.

Muhula wa masomo unaanza **tarehe …………** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **tarehe ……….** Mwisho wa kuripoti ni **tarehe …………**.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

**Vifaa na sare za shule zinapatikana shuleni au unaweza ukajishonea/kununua nyumbani**.

**2.1 Sare za shule hii ni kama ifuatavyo:**

i. Mashati mawili (2) ya rangi ya **blue bahari**, yenye **mikono mirefu** (kama inavyoonekana kwenye **Picha 1**).
ii. Sketi mbili (2) za kitambaa cha **shuka la masai** lenye **miraba ya damu ya mzee, nyeupe na blue**, mshono wa rinda box (rinda kubwa 1 katikati, marinda madogo 2 pembeni), **urefu mpaka kwenye kifundo cha mguu** (kama inavyoonekana kwenye **Picha 1**).
iii. Kwa waislamu, hijab (kijuba) nyeupe kitambaa cha **harua** isiyo na urembo.
iv. Viatu **vyeusi** vya kufunga na kamba, visigino vifupi, visivyo na urembo na visiwe buti.

v. Soksi **nyeupe** isiyokuwa na mchanganyiko wa rangi yoyote jozi.
vi. Sweta rangi ya **blue**.
vii. Nguo za kushindia (gauni) rangi ya **blue**, **kitambaa cha suti ISTEM no.1**, mshono wa **solo**, **urefu mpaka kwenye kifundo cha mguu**, mikono mirefu/mifupi ya shati.
viii. Tai, rangi ya kitambaa cha sketi (shuka la masai).
ix. Tshirt **nyeupe** yenye kola ya **blue**.
x. Tracksuit rangi ya **blue**.
xi. Raba rangi **nyeupe** au **nyeusi.**
xii. Soski **nyeusi** za michezo jozi 1.
xiii. Tshirt ya michezo (**Adidas au aina yoyote**) **nyeupe mikono mirefu**.

**Zingatia**: Kwa mwanafunzi aliyekuwa mwanachama wa skauti na anapenda kuendelea aje na sare za skauti.

**2.2 Michango ya Shule**

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na. **30701100165**, yenye jina la **Tinde Girls Recurrent** katika Benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

**Zingatia**: Kila mzazi/mlezi amkatie mwanae bima ya afya ya **NHIF** ya **Tsh. 50,400/=** kwa mwaka **au** alipe shuleni kiasi cha **Tsh. 50,400/= taslimu**. Kwa mwanafunzi ambaye tayari ana bima ya **NHIF** aje na **kadi** na mchango wa **Tsh. 50,400/=** hautamhusu.

**2.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni (pia yanapatikana shuleni) ni kama ifuatavyo:**

i) Ream ya karatasi 2 (kwa mwaka),
ii) Vitabu vya masomo ya taasusi husika (angalia orodha ya vitabu iliyoambatanishwa),
iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia,
iv) Scientific calculator kwa masomo ya sayansi na hesabu,
v) Godoro futi 2½ aina yoyote (Malaika, Victoria, Superbanco, Tanform, n.k.),
vi) Mashuka manne (4) (2 **pinki** na 2 **meupe** tu bila maua)**,**
vii) Mto 1 **(sio lazima),**
viii) Chandarua 1 cha **mviringo** na rangi yoyote,
ix) Vyombo vya chakula (sahani 1, bakuli 1, kijiko 1 na kikombe1),
x) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko,

xi) Vifaa vya usafi: **PCM**-Fyekeo/kwanja moja na brashi ngumu ya chooni moja; **HGL-**jembe moja na mpini; **HKL-**reki moja na mpini; **HGE**-mfagio wa ndani mmoja na panga moja; **HGK**-mfagio wa ndani mmoja na panga moja; **CBG**-Mfagio wa nje (chelewa) mmoja na Mopa moja; **PCB**-Mopa moja na brashi ngumu ya chooni moja; **HGLi/HGFa**-Jembe moja na mpini.

xii) Spring file (Faili la Plastiki) kwa ajili ya kutunzia taarifa za wanafunzi shuleni.

**2.4 Viambatanisho na Fomu Muhimu:**

i) Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga wa hospitali ya serikali,

ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai,

iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule,

iv) Picha nne (4) za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwanfunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu, na

**2.5 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

Rtonange

**PENDO W. MATONANGE**
**MKUU WA SHULE**

HEADMISTRESS
TINDE GIRLS HIGH SCHOOL
SHINYANGA

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; nesi wa shule na mwalimu wa malezi
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa kama simu ya mkononi, pasi (ya umeme au mkaa), radio ama kifaa chochote cha mziki.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni .
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
xviii. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yoyote yule.
xix. Kutembelea nyumba za watumishi bila kibali maalum.
xx. Kuingia ofisi za watumishi bila kibali maalum.
xxi. Kushiriki/Kusaidia kutoa mimba
xxii. Kumtesa mwanafunzi mwenzake/kumdhalilisha na kumnyima raha.
xxiii. Kugomea adhabu/kukataa adhabu.
xxiv. Kuendesha biashara ya aina yoyote shuleni.
xxv. Kukaribisha wageni bila idhini ya uongozi wa shule.
xxvi. Kulala nje ya shule bila ruhusa.
xxvii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma/mwanafunzi mwenzake.
xxviii. Kutumia vipodozi vya kuchubua ngozi (Cosmetics) kwani ni hatari kwa afya.
xxix. Kutofanya usafi katika majengo muhimu shuleni kama mabwenini, darasani, vyooni,bwaloni, ikiwemo kufagia, kupiga deki, kuondoa buibui popote zitakapo onekana na usafi wa mazingira kwa ujumla.Kutunza na kuboresha mazingira ya shule kama kupanda miti na maua kwenye ndoo.
xxx. Ni lazima wanafunzi wote wavae sare ya shule (full uniform) wakati wote wa :-
    a) Masomo darasani/siku ya vilabu vya masomo.
    b) Wanapotoka nje kwa shughuli za kishule.
    c) Mihadhara ya shule ikiwemo school baraza.
    d) Wanapoenda hospitali
    e) Kufanya kazi za nje “Extra- Curricular activities” wavae sare za kazi.
    f) Wanapoenda Kanisani/ msikitini.

g) Wanaposafiri kuja shuleni/ kwenda makwao.
h) Tracksuit ivaliwe wakati wa preparation ya usiku na sio wakati wowote.
i) Nguo za michezo zivaliwe wakati wa michezo tuu. Nguo za aina yoyote za nyumbani hazirusiwi kuvaliwa wakati wa michezo au kazi za nje, hivyo mwanafunzi asije na nguo za nyumbani.

xxxi. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo/mapumziko, isipokuwa kwa ruhusa maalum.

**Zingatia:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOPO JUU.**

**4. OFISI YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TINDE, SHINYANGA**

**MAELEZO BINAFSI / MKATABA WA MWANAFUNZI**

**A.** JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………..
KIDATO……………………………. MWAKA…………………………….
TAREHE YA KUZALIWA…………………………………MTAA /KIJIJI……………..
KATA………………………………………………………………….
TARAFA………………………………………………………………
WIALAYA…………………………………………………………
MKOA……………………………………………………………..
**B.** JINA LA BABA……………………………………………………hai/amefariki/haijulikani
**C.** JINA LA MAMA ………………………………………………...hai/amefariki/haijulikani
**D.** Mimi (jina kamili)……………………………………………………mwanafunzi wa kidato cha………tahasusi ya…………..kwa akili yangu timamu nimekubaliana na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
**E.** SAHIHI………………………………………..TAREHE…………………………………

**FOMU YA MKATABA WA MZAZI/MLEZI**
**A**. JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI……………………………………………………
**B**. MZAZI/MLEZI WA (Jina la mwanafunzi)……………………………………
**C**. ANUANI/ANAKOISHI……………………………………………………………
**D**. Mimi (Jina la mzazi/mlezi)………………………………………………………nakiri kukubaliana na sheria kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ya sekondari ya wasichan Tinde.
**E**. SAHIHI…………………………………………..TAREHE…………………..

**5. MAJINA NA PICHA ZA NDUGU/JAMAA WANNE AMBAO SHULE INAWEZA KUWASILIANA NAO NA**
**WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI.**

Jina la mwanafunzi…………………………………………….kidato………..tahasusi…………..mwaka……

i. JINA……………………………………………………..ANUANI………………………..
SIMU……………………………………UHUSIANO…………………………………

ii. JINA……………………………………………………..ANUANI………………………….
SIMU……………………………………UHUSIANO…………………………………………..

iii. JINA……………………………………………………..ANUANI………………………….
SIMU……………………………………UHUSIANO…………………………………..

iv. JINA……………………………………………………..ANUANI………………………….
SIMU……………………………………UHUSIANO…………………………………..

**6. PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT,**

**TINDE GIRLS' HIGH SCHOOL,**

**P.O.BOX 846,**

**SHINYANGA.**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

To the medical officer,

________________________

________________________

RE:___________________________________________________

Please examine the above named if she is physically and mentally fit for studies in this school. The examination should include/

the following categories:-

1. (a) Eyes_______________________________________________

(b) Ears_______________________________________________

(c) Chest______________________________________________

(d) Spleen_____________________________________________

(e) Abdomen___________________________________________

(f) Urine______________________________________________

(g) Stool examination___________________________________

(h) Blood______________________________________________

(i) Skin_______________________________________________

(j) Tuberculosis________________________________________

(k) Speech_____________________________________________

(l) Epilepsy____________________________________________

(m) Limbs (i.e. has muscle weakness)______________________

2. Pregnancy___________________________________________

3. Other serious diseases e.g. diabetes, anemia and rheumatism______________________

4. Any additional information e.g. physical defects or impairments, injections, chronic or family diseases,

etc.________________________________

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the named and consider that she is physically fit/unfit for full time studies in this school.

NAME:_____________________SIGNATURE_____________STATION_________________

Designation_________________________ Office Stamp__________________________

## 7. RANGI YA SARE ZA SHULE

Rangi na mshoni wa sare za darasani ni kama inavyoonekana kwenye picha hapo chini:




**Picha 1**

## 8. ORODHA YA VITABU

### 8.1 PHYSICS

(i) Physics for Adv. Level secondary schools. Student's book form 5 – TIE
(ii) Physics for Adv. Level secondary schools. Student's book form 6 – TIE

### 8.2 ADVANCED MATHEMATICS

(i) Advanced Mathematics form V – GDY Publication
(ii) Pure Mathematics (1 & 2) Backhouse
(iii) Advanced Mathematics (IVST SERIES) (By SHAYO)
(iv) Advanced Mathematics class X - XI (CHANDLER & BOSTOCK)

### 8.3 CHEMISTRY

(i) General Chemistry for Adv. Level secondary schools
student's book form 5 &6 – TIE
(ii) Inorganic chemistry for Adv. Level secondary schools student's book form 5 & 6 – TIE
(iii) Physical chemistry - Mzumbe boook project
(iv) Chemistry by Chande
(v) Organic Chemistry part (A & B) (Mzumbe BK project).
(vi) Organic Chemistry by Solomoni

### 8.4 BASIC APPLIED MATHEMATICS

(i) Basic Applied Mathematics form 5 by GDY Publications
(ii) Basic Applied Mathematics form 6 by GDY Publications
(iii) Basic Mathematics Review by GDY publications
(iv) Basic Applied Mathematics for Adv. Level secondary schools Student's book form 5 & 6 by TIE

### 8.5 GEOGRAPHY

(i) Pritchard M, John (1971) Practical Geography for Africa.
(ii) PT. Msabila (2007) A Comprensive Approach to Physical Geography for Secondary Schools.
(iii) Msabila, DT (2000) An Intergrated Focal Regional Study onHuman and Economic Geography.

### 8.6 BIOLOGY

(i) Biology for Adv. Level secondary schools student's bookform 5 – TIE
(ii) Biology for Adv. Level secondary schools student's bookform six – TIE

### 8.7 KISWAHILI

(i) Kamusi ya Kiswahili – Longhorn
(ii) Kiswahili shule za sekondari, kitabu cha mwanafunzi kidato cha 5 & 6– Fasihi. - TIE
(iii)Kiswahili shule za sekondari, kitabu cha mwanafunzi kidato cha 5 & 6– Fasihi. – Lugha na sarufi TIE
(iv) Haji, G, H. (1994). Kimbunga; Dar es Salaam. TUKI

(v) Khatibu, M (1988). Fungate ya Uhuru;Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press.
(vi) Mvungi, (1985). Chungu Tamu; Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.
(vii) H. J. Mwansoko Kitangulizi cha Tafsiri Nadharia na Isimu
(viii) Rboert S. (1970); Mapenzi Bora, Dsm; Evance & Brothers LTD
(ix) Hussein, E. (1988). Kwenye Ukingo wa Thim;Nairobi Oxford University Press.
(x) Mbogo, E (1993). Morani; Dar es Slaam. Dar es Salaam University Press
(xi) Mohamed, S. A (1990). Kivuli Kinaishi;Nairobi OxfordUnivestriy Press
(xii) Penina Mhando; Nguzo Mama
(xiii) Msokile, M (1990). Usiku Utakapokwisha; Dar es Salaam: Dar es Salaam Univesity Press.
(xiv) Robert, S (1967). Kufikirika; Nairobi Oxford Univesity Press
(xv) Shafi, A.S. (1997). Vuta n'Kuvute; Dar es Salam. OxfordUniversity Press.
(xvi)Tuwa, H (2007). Mfadhili; Dar es Slaam. Macmillan.

**8.8 ENGLISH LANGUAGE**

(i) Arm, A.K. (1969). The Beautiful Ones Are Not Born; New York: Colllier Macmillan.
(ii) Chinua, A. (1988). A Man of the People, Oxford: Heinemann Education Publishers.
(iii) Chinua, A. et al. (2000). Encounters from Africa. Nairobi. Macmillan Publishers Ltd.
(iv) Safo, D (1983). His Excelence The Head of State. Dar es Salaam.
(v) Ndunguru, S. N. (1999). DivineProvidence. Dar es Salaam; Mkuki na Nyota Publishers.
(vi) Ibsen, H (1967). An Enemy of the People Nairobi. Heinemen Education Books Ltd.
(vii) Imbuga, F (1976). Betrayal in The city.
(viii) Ngungi wa Thiong'o & Ngungi wa Mirii, (1982). I will Marry When I want. Nairobi
(ix) Omtatah, O. (2006). Lwanda Magere. Dar es Salaam. Mkuki naNyota Publishers.
(x) Bukenya, A (2004). Rugan. J (2005). Black Mamba. Dar es Salaam. Mkuki na Nyota Publishers.
(xi) The Bridge. Dar es Salaam. Mkuki na Nyota Publishers.
(xii) Mloka, C (2005). The Wonderful Surgeon and other Poems. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers
(xiii) Tanzania Institute of Education. (1996). Selected Poems. Dar Salaam. Tanzania Institute of Education
(xiv) Communication Skills-Jekami
(xv) Advanced Concise Dictionary

**8. 9 ECONOMICS**

(i) Principles of Economics. D.N. DWIVEDI. (Professor in Economics)
(ii) Economics for Advanced level paper one professional studies By C.M. Ambilikile. (Text books)
(iii) Economics for Advanced level paper two - professional studies by C.M Ambilikile (Text book)

**8.10 HISTORY**

(i) How Europe underdeveloped Africa - By Walter Rodney
(ii) General History of Africa - By Assa Okot
(iii) Contemporary Historical Events - Vol. I & II By Shibitali C. K Tumaini

(iv) The Revolutionary Years, West Africa Since 1800 - By Webster J. B & Boachen A. A
(v) Mastering Modern World History. - By Norman Lowe

**8.11 GENERAL STUDIES**
(i) General Studies For Secondary School - By Mbalase, R.
(ii) General Studies By SETA